KUSHEREKEHEKE A UTAKATIFU

MWONGOZO WA MAOMBI NA KUFUNGA

CHURCH OF THE NAZARENE - AFRICA REGION

www.africanazarene.org

“Yoshua akawaambia watu,
‘Jitasakeni; maana
kesho BWANA atatenda
mambo ya ajabu kati yenu’”
Yoshua 3:5

Maelezo ya Jumla

Mwaka wa 2012 umetangazwa kuwa mwaka Kusherehekea Utakatifu! Mwanzo wetu wa msisitizo utakuwa muda wa maombi na kufunga, ambao utaanza na Jumatano ya Majivu, tarehe 22 Februari 2012 na kufikia kilele na ibada ya kusherehekea Jumapili ya Pasaka, tarehe 8 Aprili 2012. Wakati huu, unaojulikana kwa wengi kama wakati wa Kwaresima, utadhihirishwa na kutakaswa kwa binafsi na kutakaswa kwa ushirika tunapojitayarisha kwa “baraka tele”.

> “Ee BWANA, nimesikia habari zako, nami naogopa, Ee BWANA, fufua kazi yako katikati ya miaka; katikati ya miaka tangaza habari yake” (Habakuki 3:2)

Wakati wa maombi na kufunga ni wakati wa kumuomba kwa Baba awashe moto wa njaa na shauku ya utakatifu katika njia ambayo haijawahi kutokea kwetu na kwa Kanisa lote la Mnazareti katika Afrika; wakati wa kumuomba Mungu awashe moto wa uamsho na kutuma baraka tele kwa watu Wake. Ni wakati wa kuombea uamsho wa mtakatifu, na kuruhusu Roho Mtakatifu atutakase na kututayarisha kuwa vyombo vyake vya kuongoza katika wakati wa kuburudisha na mavuno mengi. Wakati huu utakuwa wakati wa kujitayarisha kwa msisitizo wa Kusherehekea Utakatifu kuanzia Jumapili ya Pasaka tarehe 8 Aprili 2012 hadi Jumapili ya Pentekoste tarehe 27 Mei 2012.

Ujumbe huu umekusanywa ili kusaidia kila kanisa la mtaa wanapohusika katika wakati huu wa kujitakasa

- Maombi ya Uamsho Mtakatifu

- Msisitizo wa Kikundi cha Maombi
- Kalenda ya Maombi
- Maombi ya Kutembea
- Saa ambayo Inabadilisha Ulimwengu
- Mtindo wa Maombi ya Kilele
- Maonyesho ya Maombi na Mtindo wa Sifa

- Kufunga kwa ajili ya Uamsho Mtakatifu
  - Kalenda ya Maombi ya siku 47 za Muda wa Kwaresima kutoka Jumatano ya Majivu hadi Jumapili ya Pasaka na orodha na shughuli zilizopendekezwa za kanisa lako la mtaa na washirika wa mkutano katika kuhusika wakati wa muda wa Maombi ya Kusherehekea Utakatifu na Kufunga.
  - Maelezo ya upana na orodha inayowezekana kwa kila shughuli iliyopendekezwa.

Maombi ya Uamsho Mtakatifu

Je, Maombi ni nini?

Maombi ni kuwasiliana na Mungu. Yanahusisha kunena na Mungu na pia kusikiliza majibu yake. Maombi ni mwaliko kwa uhusiano wa ndani na Baba yetu wa Mbinguni. Inahusu hakikisho letu kwamba anatupenda mno hata Akamtuma Mwanawe wa pekee kufaa msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. Maombi ni kuitika kwetu kwa upendo huo kwa kumkaribia Mungu na kuwa na muda na Yeye (Yohana 15:9).

Je, tunapaswa kuomba kivipi?

- Amua wakati na mahali pa kuombea (Danieli 6:10)
- Njoo na Moyo ulio wazi (Waebrania 10:22)
- Omba kwa Imani (Mathayo 21:22; Yakobo 1:6)
- Omba katika Jina la Yesu (Yohana 14:13-14)

Baadhi ya Mahitaji ya Maombi:

- Sifa na Kusujudu (Zaburi 5:1-6; 1 Mambo ya Nyakati 29:11-13)
- Shukrani (Zaburi 107:1; Wakolosai 1:3)
- Toba (Mathayo 6:12-13; Yohana 1:9)
- Maombi – kumuomba Mungu akutane na mahitaji yetu (Mathayo 6:9-13; Yakobo 1:5)
- Maombi kwa ajili ya watu wengine (Wakolosai 1:3-12; Yakobo 5:13-16)

Kuombea Uamsho Mtakatifu wa Binafsi

Maombi ya Mfalme Daudi yanatufundisha jambo kubwa sana juu ya kuombea Uamsho wa Binafsi

- Alimuomba Mungu amchunguze moyo wake na kutoa dhambi zo zote zilizofichwa (Zaburi 139:23-24)
- Alikiri dhambi zake na kuomba msamaha (Zaburi 51:3-5)
- Alimuomba Mungu amsafishe kutokana na dhambi zake (Zaburi 51:7)
- Alimuomba Mungu amuumbie moyo safi na wala asimuondolee Roho wake Mtakatifu. (Zaburi 51:10-11)
- Alimuomba Mungu amponye na damu za watu (Zaburi 51:14).
- Alikubali kwamba Mungu hujibu iliyovunjika na kupondeka (Zaburi 51:17)
- Alifurahia, kwa ujasiri, katika majibu ya Mungu kwa maombi yake (Zaburi 51:18-19)

Kuomba kwa ajili ya Uamsho Mtakatifu wa Ushirika

Wakati unaombea Utakatifu wa Ushirika, kumbuka yafuatayo:

- Mungu huchukizwa na makanisa yaliyo na vuguvugu (Ufunuo wa Yohana 3:16)
- Mungu anataka kufufua makanisa yetu (Ufunuo wa Yohana 2:4-6)

- Mungu anataka kutupa Roho wake Mtakatifu zaidi (Luka 11:13)
- Achana na sanamu zote na vizuizi (Mathayo 4:8-10; Wakolosai 3:8-10)

Mambo ya Kuombea

- Omba kwamba Mungu ataumba roho iliyovunjika (Isaya 57:15; Yakobo 4:6)
- Ombea ufahamu wa ndani na tamaa ya Utakatifu Wake (Isaya 6:1-5)
- Omba kwamba Mungu atadhihirisha dhambi zote zilizojificha (Zaburi 19:12-14)
- Omba kwa ajili ya njaa ya Neno na hiari ya kuwa mtiifu (Zaburi 119:97, 103; 1 Yohana 2:3-6)
- Waombee Wachungaji wahubiri kwa nguvu na ushawishi (1 Wakorintho 2:1-4)
- Omba kwamba waumini wawe na upendo wa ndani kwa Yesu Kristo (Mathayo 22:37-38)
- Ombea ujazo wa Roho Mtakatifu (Luka 11:13; Matendo ya Mitume 1:8)

Ahadi za Mungu

- Mungu ataiponya nchi yetu (2 Mambo ya Nyakati 7:13-14)
- Mungu atatujibu tukiomba kwa mapenzi yake (1 Yohana 5:14)
- Mungu atatumwagia Roho Wake tukimuomba (Yoeli 2:28)
- Mungu atatupa ushindi (Warumi 8:37-39)

Kundi la Kusisitiza Maombi na Kalenda ya Maombi

Mkutano wote utajitoa kwa maombi na kufunga kwa ajili ya uamsho Mtakatifu kwa muda wote wa kipindi hiki. Kwa

kuongezea, kila juma tutaombea kikundi maalum ndani ya kanisa. Katika juma, kikundi hicho maalum kitakuja pamoja na kuomba, kwa ajili ya masomo na mafundisho juu ya maombi na kufunga, na kuhimizana.

- Juma la Kwanza: Wanawake
- Juma la Pili: Wanaume
- Juma la Tatu: Watu Wazima
- Juma la Nne: Vijana
- Juma la Tano: Watoto
- Juma la Sita: Maombi ya Pamoja

Kila juma la **Kalenda ya Maombi** limeelezewa na mtazamo wa maombi ya eneo la jimbo na mambo yanayotiliwa mkazo ambayo tunapitia kwenye bara letu leo. Tumia Kalenda ya Maombi kupanga matukio ya maombi na kufunga. Kumbuka kwamba maombi yetu ya kwanza wakati wa kipindi hiki ni uamsho wa Utakatifu katika Afrika yote.

Maombi ya Kutembea[1]

Je, Maombi ya Kutembea ni nini?

“Maombi ya kutembea ni kuomba katika sehemu ambazo unatarajia Mungu kuyajibu maombi yako.” (Je, Yesu Angeomba Nini”, na Way Makers)

Ni maombi ya maombezi katika sehemu zile zile ambazo unamtafuta Mungu kufanya kazi. Muktadha wa maombi ya kutembea humleta mtu anayeomba katika mawasiliano ya ana kwa ana na watu wa jamii ambao unawaombea kwa moyo wa hiari.

Je, Maombi Haya yanafanyaje Kazi?

Maombi ya kutembea ni kuenenda peke yako au katika vikundi, katika sehemu zilizotengwa au jamii, na kuombea mahitaji ya

watu ambao wanaishi sehemu hizo. Maombi haya yanatuwezesha kuomba katika sehemu zilizofungwa kwa wale walio katika jamii ambao wanahitaji maombi yetu.

Maombi ya Kutembea ni kuomba kwenye ____

- Maombi ya kutembea ni kuomba kwa niaba ya wengine.
- Maombi ya kutembea ni kusonga karibu na _____ kwa wale unaowaombea ili uweze kufahamu vyema mahitaji yao na jinsi ya kuyaombea. Maombi haya yanawezesha moyo wako kutambua mahitaji yaw engine na kuweka moyo wako katika hali ya moto _____ kiroho ambayo tunahitaji na kutendeka.
- Maombi ya kutembea husaidia kukufanya uwe mwepesi kwa jambo lenyewe, sauti kuona, na harufu husaidia kuhusisha roho wako katika maombezi. _____

Maombi ya kutembea ni kuomba na utambuzi

- Ni utambuzi wa kuitika. Yale uanayoombea yako mbele yako.
- Ni utambuzi uliochunguzwa. Ni kuomba na maarifa ya historia ya sehemu au jamii ambapo unaombea.
- Ni utambuzi uliovumbuliwa. Tunahitaji kuomba na kumuomba Mungu avumbulie mahitaji tunayohitaji kuangazia tunapoomba. Tunahitaji kumruhusu Roho Mtakatifu atuongoze tunapoomba.

Maombi ya Kutembea kwa Vitendo

1. Omba na mwenzi au na kikundi
2. God's desire Omba na kusudi – mapenzi ya Mungu

3. Kuomba na Neno la Mungu – kuomba ahadi za Mungu zaidi ya matatizo
4. Omba na Roho wa Mungu
5. Sikiliza na umchunguze Mungu

Saa Inayobadilisha Ulimwengu[2]

Mviringo wa maombi hapa chini umeundwa ili kusaidia kuanganzia wakati tunaomba. Unagawa lisaa limoja katika dakika tano za maombi ya aina tofauti. Baada ya dakika tano, badilisha kwa mtindo mwingine wa maombi. Mtindo huu utakuwezesha kuwa na muda unaofaa katika maombi ya Uamsho Mtakatifu katika Jimbo lote la Afrika.

1. Sifa na kuabudu
2. Kumngojea Bwana
3. Kukiri kwa hatia na dhambi
4. Kuomba Maandiko
5. Kutazama
6. Maombezi
7. Maombi ya huruma
8. Shukrani
9. Wimbo
10. Kukakiriri
11. Kusikiliza
12. Sifa

[1] *Diagram designed by Dick Eastman, originator of the Change the World School of Prayer*

Mtindo wa Kilele cha Maombi

Kilele cha maombi ni jitihada ya maombi ya pamoja ambapo unaalika makanisa mengine mnayoshirikiana nayo, madhehebu, viongozi wa jumuiya na kadhalika, ili kuja pamoja kuombea masuala muhimu katika jumuiya, lakini kwanza ni mimiminiko wa Roho Mtakatifu.

Ratiba Iliyopendekezwa

A. Karibu
   1. Zaburi 42:1-2; 84:1-2: 10-11; 133:1-3
   2. Maelekezo

3. Maombi ya maandilizi: kikundi cha watatu. Kila kikundi kishirikia kwa dakika moja mahitaji yenu muhimu na kuombea kila mmoja ili kuweka wazi mizigo ya mioyo yenu na mjitayarishe kuwa na mtazamo kwa wengine na jumuiya yenu.
4. Sifa: Zaburi 132
5. Nyimbo za kuabudu

B. Toba na kutakaswa kwa binafsi.

Maandiko: Yoeli 2:12-14

1. Waulize watu kadhaa kuomba kwa ajili ya mwelekeo, ulinzi, na kuthihirishwa kwa uwepo wa Mungu.
2. Nyimbo za Kuabudu
3. Soma Yakobo 4:8-10. Tumia muda wa maombi ya kipekee kwa ajili ya hali yako ya kiroho.

C. Ombea mahitaji maalum katika jumuiya

Maandiko: 2 Mambo ya Nyakati 7:14

1. Waalike Viongozi mashuhuri kuja mbele na kuombea masuala ya mbele katika jumuiya yako.
2. Soma Yoeli 2:28. Ombea mmiminiko wa Roho Mtakatifu katika jumuiya yako.

D. Miviringo ndogo ya Maombi

1. Wakusanye wanaume na wanawake pamoja
2. Shiriki mahitaji pamoja. Wachungaji pia huumia kutokana na ukosoaji, ukosefu wa kujitoa kwa washirika, mashindano, na uoga ya kufanya makosa. Msijadili maombi
3. Zunguka mviringo na kila mtu anayemuombea mtu aliye upande wake wa kushoto/kuume mpaka kila awe na nafasi ya kuomba na mtu mwingine pia amemuombea.

E. Maombi ya Mlima Yanayosonga Haraka

Maandiko: Yeremia 33:1-11

1. Ombea washirika wa familia: wazazi/babu na bibi, ombea watoto walioopotea.
2. Ombea ndoa ziookolewe, zirejeshwe; kukiri na toba; mabadiliko ya nia.
3. Ombea makanisa yawe nyumba za maombi kwa mataifa yote; washirika wa halmashauri, viongozi

F. Ufufuo, Kufanywa Upya

Maandiko: Matendo ya Mitume 3:19; Ezekieli 37; Zaburi 85:6

1. Ombea mada ya Maandiko juu ya ufufuo, kufanywa upya, mmiminiko mpya wa Roho Mtakatifu.
2. Alika viongozi wapya wa kizazi chini ya umri wa miaka 40 kuja mbele na kupiga magoti; wazingire na maombi kwa ajili ya kufanywa upya.

G. Maombi ya Sifa na Shukrani

Maandiko: 1 Mambo ya Nyakati 29:11-13, Zaburi 95:1-6, Zaburi 100

1. Kusanyika kwa watu watatu. Mshukuru Mungu kwa yale ametenda katika siku na saa.

Maonyesho ya Maombi na Sifa

Maonyesho ya Maombi na Sifa ni wakati ambapo mkutano huja pamoja kusoma Maandiko, kuimba nyimbo, kushuhudia kuhusu maombi yaliyojibiwa, kuhimizana.

Ratiba hii inapaswa kutayarishwa mbele.

Nyimbo za Maandiko, na shughuli zingine zinapaswa kupewa watu tofauti ili kuwe na watu tofauti wanaoongoza ibada.

Ifuatayo ni mfano wa Maonyesho ya Maombi na Sifa. Hata hivyo, Ratiba zinaweza kutengenezwa kulingana na muktadha.

Maonyesho ya Mtindo wa Maombi

- ***Gawa mwongozo kwa viongozi wahusika waliochaguliwa mapema ili kutayarisha kuongoza mkutano.***
- ***Chagua viongozi wengi na wasomaji iwezekanavyo.***

- ***Tafadhali fuata maneno juu ya maombi hapo chini.***
- ***Tafadhali soma Maandiko yote kutoka kwa Tafsiri Mpya ya Kimataifa (NIV)***

Mchungaji au Kiongozi wa Ibada: Karibu katika nyumba ya maombi kwa mataifa yote. “Nyumba yangu itaitwa nyumba ya sala kwa mataifa yote” (Marko 11:17).

Kiongozi wa Ibada: Nyimbo za Sifa na Ibada – dakika 15: Nyimbo zilizopendekezwa: Hapa nipo Kukuabudu; Njoo Ee Mfalme.

Maombi ya Sifa na Ibada

Kiongozi A: Soma Zaburi 96

Imbeni Pamoja: Utukufu, Haleluyia

Omba maombi ya Sifa, Ibada na Shukrani

Maombi ya Kufikiria na Kukiri

Kiongozi B: Soma 2 Wakorintho 7:1

Imbeni Pamoja: Mapenzi Yako Yafanyike.

Tafadhali piga magoti karibu na kiti chako kwa wakati kufikiria, na maombi ya kukiri na toba.

Maombi ya Uamsho Mtakatifu.

Kiongozi C: Soma Habakuki 3:2

Imbeni Pamoja: Andaa Njia

Ingieni katika vikundi vya watatu hadi watoto na muombee Uamsho wa Utakatifu kwenye Jimbo la Afrika

Maombi ya Maombezi.

Kiongozi D: Soma Zekaria 4:6

Imbeni Pamoja: Mbele Ninaendelea

Omba kwa vikundi vya watatu hadi watano.

Maombi kwa Wasiookoka

Kiongozi E Soma Zaburi 2:7-8

Imbeni Pamoja: Tuma Nuru

Lieni kwa pamoja kwa niaba ya wale wasiomjua Yesu Kristo kama Mwokozi wao.

Maombi ya Familia

Kiongozi F: Soma Mwanzo 18:19; Kumbukumbu la Torati 6:6

Imbeni Pamoja: Yuaishi

Mwe katika vikundi vya wawili na uombee familia ya kila mmoja.

Maombi ya Uponyaji

Kiongozi G: Soma Kutoka 15:26b

Imbeni Pamoja: Mimi ni Bwana Akuponyaye

Ninawaalika wale walio na mahitaji ya afya waje mbele waombewe, na wengine wajiunge kwa kuwaombea

Maombi ya Shukrani

Kiongozi H: Soma Zaburi 100

Imbeni Pamoja: Mungu Mtukufu

Ombeni pamoja maombi ya umoja ya shukrani na utukufu.

Ombea Maeneo ya Afrika na Jimbo.

Kiongozi A

Sasa, tutaombea kila moja ya maeneo saba katika jimbo letu. Tunaanza na Eneo la Afrika ya Kati na Afrika Mashariki. Mkurugenzi wetu wa Eneo la Kati ni Kasisi Paul Mtambo. Mkurukenzi wa Eneo la Mashariki ni Kasisi Don Gardner.

Ninawaalika ninyi wote msimame pamoja. Hebu tusome Zaburi 96:2-3 pamoja (ikionyeshwa kwenye pazia): “Mwimbieni Bwana, libarikini jina lake; tangazeni wokovu wake siku kwa siku. Wahubrini mataifa habari za utukufu wake, na watu wote habari za maajabu yake” (Zaburi 96:2-3)

Namhimiza kila mtu aliye upande wa mkono wangu wa kuume kuunda miviringo kidogo pamoja wa kuombea Eneo la Kati pamoja na Kasisi Mtambo, wasimamisizi wa wilaya na wachungaji. Watu walio kwenye mkono wangu wa kushoto, tafadhli tengenezeni mviringo kidogo wa kuombea Eneo la Mashariki pamoja na Kasisi Gardner, msimamizi wa wilaya na wachungaji.

Omba baadhi ya mada hizi za kila eneo: dhihirisho la uwepo wa Mungu, uinjilisti, ufanyaji wa uanafunzi, utakatifu, maendeleo ya kanisa, wilaya na viongozi, upanuaji wa mikakati ya misheni, uwakili wa kafara, na kufanywa upya thabiti katika Roho.

Sasa, ninaalika vikundi vidogo viombe kwa dakika mbili. Wakati kuimba kunaanza, tafadhali funga wakati wako wa maombi.

Imba: Hizi ni Siku za Eliya

Kiongozi B: Tunaendelea kuomba, na kuangazia Eneo la Pembe la Afrika na Eneo la Ufaransa. Mkurugenzi wetu wa Eneo la Pembe la Afrika ni Kasisi Ermias Choliye. Mkurugenzi wetu wa Eneo la Ufaransa ni Kasisi Dkt Paulo Sueia.

Ninawaalika ninyi wote msimame pamoja. Acha tusome Zaburi 22:27-28 pamoja (ikionyeshwa kwenye pazia): “Miisho yote ya dunia itakumbuka, na watu watamsujudia. Maana ufalme una BWANA, Naye ndiye awatawalaye mataifa” (Zaburi 22:27-28).

Ninawahimiza watu walio upande wangu wa **kuume** waunde miviringo ndogo ya kuombea Eneo la Pembe la Afrika na Kasisi Choliye, wasimamizi wa wilaya na wachungaji. Watu walio kwenye mkono wangu wa kushoto, tafadhali tengenezeni mviringo wa kuombea Eneo la Ufaransa pamoja na Kasisi Sueia, wasimamizi wa wilaya na wachungaji.

Omba baadhi ya mada hizi za kila eneo: dhihirisho la uwepo wa Mungu, uinjilisti, ufanyaji wa uanafunzi, utakatifu, maendeleo ya kanisa, wilaya na viongozi, upanuaji wa mikakati ya misheni, uwakili wa kafara, na kufanywa upya thabiti katika Roho.

Sasa, ninaalika vikundi vidogo viombe kwa dakika mbili. Wakati kuimba kunaanza, tafadhali funga wakati wako wa maombi.

Imbeni: Siku za Kale

Kiongozi C: Tunaendelea kuomba, na kuangazia Eneo la Katikati na Eneo la Afrika Magharibi. Mkurugenzi wetu wa Eneo la Katikati la Afrika ni Kasisi Chanshi Chanda. Mkurugenzi wetu wa Eneo la Ufaransa ni Kasisi Mark Louw.

Ninawaalika wote tusimame. Hebu tusome mathayo 24:14 kwa pmaoja kutoka kwa pazia: “Tena habari njema ya ufalme itahubiriwa katika ulimwengu wote, kuwa ushuhuda kwa mataifa yote, hapo ndipo ule mwisho utakapokuja” (Mathayo 24:14).

Ninawahimiza watu walio upande wangu wa **kuume** waunde mviringo ndogo ya kuombea Eneo la Katikati la Afrika na Kasisi Chanda, wasimamizi wa wilaya na wachungaji. Watu walio kwenye mkono wangu wa **kushoto,** tafadhali tengenezeni mviringo wa kuombea Afrika Magharibi pamoja na Kasisi Louw, wasimamizi wa wilaya na wachungaji.

Omba baadhi ya mada hizi za kila eneo: dhihirisho la uwepo wa Mungu, uinjilisti, ufanyaji wa uanafunzi, utakatifu, maendeleo ya kanisa, wilaya na viongozi, upanuaji wa mikakati ya misheni, uwakili wa kafara, na kufanywa upya thabiti katika Roho. Ombeni kwa dakika mbili, funga wakati uimbaji utaanza.

Imbeni: Mpigieni Bwana Kelele

Kiongozi D: Tutafunga kwa maombi ya Eneo la Kusini na Ofisi ya Jimbo, mkurugenzi wa Eneo la Kusini ni Kasisi Collin Elliott. Msimamizi wa Jimbo, Dkt Filimao Chambo, anaongoza kanisa katika jimbo lote. Tafadhali tengenezeni miviringo ndogo mahali mlipo, na mjitayarishe kuomba pamoja kwa sauti.

Ninawahimiza watu walio upande wangu wa **kuume** waunde miviringo ndogo ya kuombea Eneo la Afrika Kusini na Kasisi Elliott, wasimamizi wa wilaya na wachungaji. Watu walio kwenye mkono wangu wa **kushoto**, tafadhali tengenezeni

mviringo wa kuombea Ofisi ya Jimbo na Dkt Filimao Chambo pamoja na kundi lake, wasimamizi wa wilaya na wachungaji.

Kisha ombea Msimamizi fulani wa Wilaya, wachungaji wa wilaya, na mchungaji wako.

Omba baadhi ya mada hizi za kila eneo: dhihirisho la uwepo wa Mungu, uinjilisti, ufanyaji wa uanafunzi, utakatifu, maendeleo ya kanisa, wilaya na viongozi, upanuaji wa mikakati ya misheni, uwakili wa kafara, na kufanywa upya thabiti katika Roho.

Sasa, ninaalika vikundi vidogo viombe kwa dakika mbili. Wakati kuimba kunaanza, tafadhali funga wakati wako wa maombi.

Baada ya wimbo, uko huru kwenda kwa ushirika (wakati wa chakula cha mchana ikiwa inawezekana) na maono na shauku iliyofanywa upya kwa misheni yetu ya kuwafanya wanafunzi kama Kristo katika mataifa tukianzia Afrika.

Imbeni: Anatawala

Kiongozi wa Ibada: Kuanzishwa kwa kibodi “Mwabudu Mfalme”

Funga kwa ajili ya Uamsho wa Utakatifu

“Takaseni saumu,
iteni kusanyiko la dini,
Wazee na wakusanye
wenyeji wote wa nchi;
Waende nyumbani kwa BWANA,
Mungu wenu, na
kumlilia BWANA.”
Yoeli 1:14

Je, Kufunga ni Nini?

Kufunga ni kula kiasi au kujitenga na chakula, aidha kutokana na haja au tamaa.

Kufunga ni nidhamu ya kiroho ambayo ilianza wakati Agano la kale. Kisa cha kwanza cha kufunga ambacho tunakiona katika Biblia kimerekodiwa katika Kutoka 34:27-28, “BWANA akamwambia Musa, ‘Andika maneno haya; kwa kuwa mimi nimefanya agano nawe, na pamoja na Israeli, kwa mujibu wa maneno haya. Naye alikuwa huko pamoja na BWANA siku arobaini na masiku yake; hakula chakula, wala hakunywa maji, Naye akaandika katika hizo mbao, hayo maneno ya maagano, hizo amri kumi.”

Yesu alifunga siku arobaini nyikani kabla ya kujaribia na ibilisi (Mathayo 4:1-11), na akadhihirisha jinsi tunavyoweza kushinda majaribu makubwa ambayo ibilisi huweka katika njia zetu kwa kujua, kuamini katika, na kukariri Neno la Mungu.

Kuna marejeleo mengi juu ya kufunga katika Biblia, kama vile Luka 2:36-37, Matendo ya Mitume 13:1-3, na Matendo ya Mitume 14:23.

Kufunga kwa kiroho kunahusisha kuweka kando shughuli na pia

kupunga kula kwa chakula na kubadili shughuli hizi na mazoezi ya maombi na kujihusisha na mambo ya kiroho.

Aina tatu za kufunga zinatambuliwa: *kawaida*, ambapo hakuna kula chakula kwa muda fulani, ingawa kunaweza kuwa na vinywaji; kufunga kwa kiasi, ambapo mankuli yanakuwa kidogo, ingawa chakula kidogo kinaruhusiwa; na kufunga kwa kamili, ambapo kuna kuepukana kabisa na chakula na vinywaji vya aina yo yote.[3]

Kufunga kwa ajili ya vitu mbali na chakula inaweza kuhusisha kujitenga na starehe na kusoma, kuchagua muda wa kuwa peke yako na kimya ili kutafuta uso wa Mungu, kujitenda na uhusiano wa kimapenzi.

- Kufunga kwa uamsho wa kiroho kunapaswa kuwa kila wakati kunaambatana na maombi, kukiri kwa dhambi, kusoma neno la Mungu (Zaburi 51:1-13, Zaburi 119:9-16)
- Kufunga kunapaswa kufanywa kwa unyenyekevu wa roho (Isaya 58:5)
- Kufunga kunapaswa kufanywa na moyo ulio wazi na lengo kuu la kumtukuza Mungu (Mathayo 6:16-18).
- Kufunga kunapaswa kufanywa na moyo wa Furana na uliojaa Shukrani (Mathayo 6:17-18)
- Kufunga kunapaswa kuambatana na utiifu kwa amri za Mungu (Isaya 58)
- Njia nyingine ya kujitenga na umakini wetu na mahitaji yetu na tamaa ni kuangazia wengine na kukutana na mahitaji yao wakati wa kufunga (Isaya 58:6-7)

Baadhi ya Miongozo ya Kufunga

- Watu wengine hupata ikiwa rahisi kuingia katika kufunga. Anza kwa kujitenga na chakula kimoja, na uongeze muda wako wa kufunga pole pole.
- Watu walio na ugonjwa usiopona kama vile Ugonjwa wa Sukari wanapaswa kushauriana na muuguzi wao kabla ya kuanza kufunga.

- Watoto wadogo wanaweza kufunga kwa kujitenga na starehe, vitu vyao vya kucheza na hata pipi kwa muda fulani
- Panga mikutano ya maombi na vikundi vya masomo ya Biblia wakati wa kipindi cha kufunga ili kuhimiza kila mmoja.
- Panga kukamilisha maombi ya kufunga pamoja kwa kushiriki meza ya Bwana na chakula chepesi baadaye.
- Usile sana baada ya kipindi cha kufunga kwa sababu mfumo wa vimbia utahitaji muda wa kuzoea chakula tena.
- “Kupokea baraka nzuri zaidi za Mungu kutoka kwa kufunga inahitaji kujitoa imara: Kupanga muda maalum kila siku na Mungu ni muhimu sana katika kupokea mawasiliano ya karibu na Baba. Ni lazima ujitoe mwenyewe katika kutafuta uso wa Mungu, hata (na hasa) katika wakati ambapo unajihisi mdhaifu, mlegevu, au kuchukizwa. Soma Neno lake na uombe wakati wa chakula. Tafakari juu Yake wakati unaamka usiku. Mwimbie nyimbo za sifa wakati unatamani”. (Dkt Bill Bright, Mwongozo Wako Binafsi wa Kufunga na Kuomba)

Mwongozo wa Maombi na Kufunga ulioundwa na Kasisi Samantha Chambo, Mkurugenzi wa NMI Jimbo la Afrika

Sisitizo la Kusherehekea Maombi ya Utakatifu na Kufunga pamoja na Shughuli Zilizopendekezwa

Jumatatu	Jumanne	Jumatano	Alhamisi	Ijumaa	Jumamosi	Jumapili
20 **Sisitizo la Maombi** **Kila Juma**	**21** Februari	**Jumatano ya Majivu 22** Kundi ndogo Mkutano wa maombi	**23**	**24**	**25**	**26** **Kufunguliwa rasmi kwa** **Hatua ya Kusherehekea** **Utakatifu**
27 Eneo la Afrika Kusini Ofisi ya Jimbo la Afrika **Kikundi**: Wanawake	**28**	**29** Kundi ndogo Mkutano wa maombi	**1** Machi	**2** Maombi ya Usiku Mkutano wa maombi	**3**	**4** Maonyesho ya Maombi na Sifa
5 Eneno la Katikati la Afrika Kituo cha Huduma cha Kimataifa **Kikundi**: Wanaume	**6**	**7** Kundi ndogo Mkutano wa maombi	**8**	**9**	**10** Kilele cha Maombi	**11**
12 Eneo la Ufaransa la Afrika Eneo la Kati la Afrika **Kikundi**: Watu Wazima	**13**	**14** Kundi ndogo Mkutano wa maombi	**15**	**16** Maombi ya Usiku Mkutano wa maombi	**17** Maombi ya Kutembea	**18**
19 Pembe ya Eneo la Afrika Eneo la Afrika ya Magharibi **Kikundi**: Vijana	**20**	**21** Kundi ndogo Mkutano wa maombi	**22**	**23**	**24**	**25**
26 Eneno la Afrika Mashariki iWaasiriwa wa UKIMWI na Baa la njaa **Kikundi**: Watoto	**27**	**28** Kundi ndogo Mkutano wa maombi	**29**	**30** Maombi ya Kutembea	**31**	**1** Aprili
2 Mmiminiko wa Roho Mtakatifu katika Afrika Yote na Ulimwengu wote **Kikundi**: Vyote	**3**	**4** Vikundi vidogo Mkutano wa maombi	**5**	**6** **Ijumba ya Pasaka** Chemba ya Maombi, Kambi ya Maombi	**7**	**8** **Jumapili ya Pasaka** **Ibada ya Kusherehekea**